**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA FEDHA

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA UNUNUZI WA UMMA**

Public Procurement Regulatory Authorit

*Unapojibu tafadhali taja*:

**Kumb. Na: FA.75/192/01/A/14** **26 Juni, 2026**

Kwa Taasisi Nunuzi Zote,
**Tanzania Bara.**

Yah: **WARAKA NA. 4 WA MWAKA 2025/2026 KUHUSU UTENGAJI WA ASILIMIA THELATHINI (30%) YA MPANGO WA UNUNUZI WA MWAKA WA TAASISI KWA AJILI YA MAKUNDI MAALUM**

---

Tafadhali rejeeni kichwa cha habari hapo juu.

**2.** Kwa mujibu wa kifungu cha 64 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410, Taasisi Nunuzi zinatakiwa kutenga sehemu ya mpango wa ununuzi wa mwaka kwa ajili ya Makundi Maalum, ambayo ni wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu, ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika fursa za ununuzi wa umma.

**3.** Aidha, Kanuni ya 35 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2024, Tangazo la Serikali Na. 518, inazitaka Taasisi Nunuzi kutenga asilimia thelathini (30%) ya ununuzi wa kila mwaka wa bidhaa, kazi za ujenzi na huduma kwa ajili ya Makundi Maalum yaliyopo katika maeneo yao.

**4.** Kwa kuzingatia Kanuni ya 35(4), Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma iliandaa Mwongozo wa Ushiriki wa Makundi Maalum katika Ununuzi wa Umma, 2026 unaoainisha taratibu za ununuzi, aina ya zabuni zinazoweza kutengwa kwa Makundi Maalum, pamoja na namna ya kutekeleza utaratibu huo kwa mujibu wa Sheria na Kanuni.

**5.** Mamlaka inapenda kuzijulisha Taasisi Nunuzi zote nchini kuwa, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imeendelea kuwezesha usajili wa Makundi Maalum kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST). Hadi sasa, idadi kubwa ya Makundi Maalum yamesajiliwa kwenye mfumo huo, hivyo Taasisi Nunuzi zinapaswa kutumia taarifa zilizopo NeST kubaini Makundi Maalum yanayopatikana na

kuyashirikisha katika fursa za ununuzi wa umma kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Mwongozo husika.

**6.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria, Kanuni na Mwongozo tajwa, Mamlaka inaelekeza Taasisi Nunuzi zote nchini kutekeleza yafuatayo:

i) Kutenga asilimia thelathini (30%) ya mpango wa ununuzi wa kila mwaka wa bidhaa, kazi za ujenzi na huduma kwa ajili ya Makundi Maalum;

ii) Kuhakikisha fursa zilizotengwa kwa Makundi Maalum zinaainishwa bayana kwenye Mpango wa Ununuzi wa Mwaka na kutekelezwa kupitia Mfumo wa NeST;

iii) Kuhakikisha zabuni zinazotengwa kwa Makundi Maalum zinazingatia uwezo, aina ya kazi, bidhaa au huduma husika, pamoja na mazingira ya soko katika eneo husika; na

iv) Kuhakikisha zabuni zilizotengwa kwa ajili ya Makundi Maalum zinatekelezwa kwa kuzingatia Mpango wa Ununuzi wa Mwaka ulioidhinishwa, Sheria, Kanuni na Mwongozo husika.

**7.** Mamlaka inazikumbusha Taasisi Nunuzi zote kuwa, kwa mujibu wa Kanuni ya 35(5) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2024, Afisa Masuuli atakayeshindwa kutenga asilimia thelathini (30%) ya ununuzi wa kila mwaka kwa ajili ya Makundi Maalum atawajibika kwa hatua za kinidhamu kwa mamlaka husika. Hivyo, Wakuu wa Taasisi Nunuzi zote wanapaswa kuhakikisha kuwa matakwa ya Sheria, Kanuni, Mwongozo husika na Waraka huu yanatekelezwa kikamilifu.

**8.** Nawatakia utekelezaji mwema.

Dennis K. Simba
**<u>MKURUGENZI MKUU</u>**